

Muhtasari wa mradi wa RIB.

Muhtasari huu umetafsiriwa kwa lugha kadhaa. Katika kurasa zetu kwenye mtandao wa intaneti utapata kwamba hazija tafsiriwa kwa sababu ukitaka kufanikiwa katika biashara yako hapa Uingereza ni muhimu sana uelewe Kiingereza vizuri.

Mbona Wakimbizi waingie kwenye biashara?

Wakimbizi wana nafasi chache sana za kupata kazi, ikihesabiwa, wana nafasi sita chini zaidi ya mtu asiye mkimbizi kufanikiwa kupata kazi. Hii ni hasara kubwa kupoteza ujuzi walionao na maarifa pia. Kwa hiyo njia mojawapo za kujiendeleza ni kufungua biashara au kuanzisha utendaji kazi ambao utafaidi jamii.

Kama tu ingekuwa rahisi hivyo?

Kama makundi mengi yasiyojiweza, wakimbizi ambao wanataka kuanzisha biashara wanakabiliwa na matatizo kadha wa kadha. Vizuizi vinavyowakabili ni kama; kukosa kutambuliwa kwa vyeti vyao, kupata mikopo ya biashara, lugha, kupata taarifa sawa, kubaguliwa, kushukiwa na kukosa kuelewa mitindo ya kufanya biashara Uingereza.

Mashirika ya Wakimbizi katika jamii hayana ujuzi wa kutosha hata wa biashara na pia wanakosa wataalam na washauri wa kibiashara ambao wanaelewa vizuri, vizuizi vya kibiashara ambavyo vinaweza kuwasumbua wakimbizi. Kwa hiyo pia inakuwa vigumu kwao kutoa usaidizi unaofaa.

Wakimbizi katika Biashara: ilianzishwa kukabiliana na matatizo kama haya. Lengo lake haswa ni:

Kutoa usaidizi wa muda mrefu kwa wakimbizi wanao taka kuanzisha biashara .

Mtandao wa Intaneti kwa Wakimbizi katika Biashara.

Mtandao huu umeleta pamoja taarifa kuhusu ushauri, mifano ya biashara, miongozo na vifaa vya mafunzo.

Miongozo ya Kujisaidia Kuanzisha biashara.

Hii itakuwezesha kuamua kama wewe wafaa kufanya biashara na vile ya kuanzisha biashara yako.

Vifaa vya Masomo kwa Washauri walio na ujuzi.

Vifaa hivi vinashughulikia historia za wakimbizi na kile mshauri wa biashara anahitaji kujua anapomsaidia mkimbizi kuanzisha biashara yake.

Vifaa vya Elimu kwa mashirika ya Wakimbizi.

Vifaa hivi vinashughulikia ushauri wa kawaida katika biashara na pia kusaidia katika kupata na kufanya kazi na washauri wa biashara wenye ujuzi.

Mafunzo.

Mradi huu utakuwa ukifanya majaribio ya mafunzo ambayo yanafaa katika ushauri wa kawaida katika biashara, kujulisha kuhusu hali ya wakimbizi na uanzishaji wa biashara na wakimbizi watendaji.

Tunatumaini kwamba mtandao huu wa intaneti utakusaidia. Tafadhali wasiliana nasi kama una maoni yoyote yale.